JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUMEYA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI
(LIMERUDIWA)

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni taasisi huru ya umma na inayojitegemea iliyoanzishwa chini ya Ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Pili ya Sheria yenye majukumu ya kuhakikisha kuwa haki za binadamu na utawala zinakuzwa, kulindwa na kuheshimiwa nchini.

Kamati ya Uteuzi inawaalika **raia wa Tanzania wenye sifa zinazotakiwa** kuwasilisha maombi kwa nafasi ya **Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna** ili kujaza nafasi zilizo wazi katika Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

A. MWENYEKITI WA TUME (NAFASI 1)

SIFA ZA KITAALUMA
Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa za kumwezesha kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au Jaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

UZOEFU UNAOHITAJIKA
Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

a) Maarifa, uzoefu na ushiriki unaoridhisha katika masuala ya sheria, utawala, siasa au mambo ya kijamii;

b) Mwenye kuheshimika kimaadili, mwaminifu, asiyekuwa na upendeleo na mwenye weledi katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora;

c) Mtu anayejitolea kwa kiwango cha juu kuhakikisha utekelezaji wa kanuni na misingi ya haki za binadamu;

d) Uwezo wa kuandika na kuwasiliana kwa ufasaha katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili;

e) Uwezo wa kuweka usawa na kufanya maamuzi ya haki na sahihi kwa haraka na kuwa na uwezo wa kuyaelezea maamuzi kwa maandishi au kuzungumza;

f) Uwezo wa kumudu masuala magumu yanayoleta (yenye) hisia na changamoto kwa kutumia mbinu sahihi na njia za kidiplomasia;

g) Uwezo wa kushughulikia masuala na malalamiko nyeti kijamii na kisiasa kwa usiri, pale inapohitajika;

h) Ujuzi mkubwa wa kutatua migogoro; na

i) Uwezo wa kufanya kazi vizuri kama sehemu ya timu, au kama mtu binafsi (akiwa peke yake).

MAJUKUMU

a) Kusimamia utekelezaji wa sera na mwelekeo wa kimkakati wa Tume;

b) Kubainisha na kugawa majukumu kwa Makamishna;

c) Kusikiliza malalamiko nyeti kuhusu uvunjifu mkubwa wa usimamizi wa kiutawala na ukiukwaji wa haki za binadamu;

d) Kuthibitisha na kupitisha maamuzi yaliyoandikwa na Makamishna na watumishi wa Tume kwa ajili ya kuhakikisha usahihi na ubora wa maudhui ya maamuzi hayo;

e) Pale inapowezekana, kutatua migogoro mahsusi kwa kutumia mbinu mbadala za utatuzi wa migogoro kama vile usuluhishi na upatanishi;

f) Kupitisha programu za kielimu zilizoandaliwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma na uelewa wa masuala ya haki za binadamu na haki za kiutawala;

g) Kusimamia uandaaji na uchapishaji wa ripoti za kila mwaka za Tume, nyenzo za kielimu na taarifa maalumu kimaudhui;

h) Kushiriki mara kwa mara kama mwezeshaji katika warsha, mikutano na semina zinazoandaliwa na kuendeshwa na Tume kwa makundi maalumu; na

i) Kuwa Msemaji wa Tume na kuiwakilisha Tume katika warsha, makongamano, na mikutano ya kitaifa na kimataifa kuhusu haki za binadamu na usimamizi wa haki za kiutawala.

]

KITUO CHA KAZI

DODOMA

B. MAKAMU MWENYEKITI (NAFASI 1)

SIFA ZA KITAALUMA
Mwombaji anatakiwa kuwa na walau Shahada ya kwanza katika mambo ya sheria, haki za binadamu, utawala, siasa au masuala ya jamii.

UZOEFU UNAOHITAJIKA
Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zinazolingana na sifa na uzoefu unaohitajika kwa ajili ya nafasi ya Mwenyekiti au Makamishna wa Tume.

MAJUKUMU
a) Makamu Mwenyekiti ataripoti kwa Mwenyekiti na atamsaidia Mwenyekiti kufanya jukumu lolote atakapangiwa na Mwenyekiti.

b) Kukaimu nafasi ya Mwenyekiti pale ambapo Mwenyekiti hatakuwepo.

KITUO CHA KAZI
DODOMA

C. MAKAMISHNA WA TUME (NAFASI 5)

SIFA ZA KITAALUMA
Mwombaji anatakiwa kuwa na walau Shahada ya kwanza katika mambo ya sheria, haki za binadamu, utawala, siasa au masuala ya jamii.

UZOEFU UNAOHITAJIKA
Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:
a) Maarifa, uzoefu na ushiriki unaoridhisha katika masuala ya sheria, utawala, siasa au mambo ya kijamii;

b) Mwenye kuheshimika kimaadili, mwaminifu, asiyekuwa na upendeleo na mwenye weledi katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora;

c) Mtu anayejitolea kwa kiwango cha juu kuhakikisha utekelezaji wa kanuni na misingi ya haki za binadamu;

d) Uwezo wa kuandika na kuwasiliana kwa ufasaha katika lugha ya Kiingereza na Kiswahili;

e) Uwezo wa kuweka usawa na kufanya maamuzi ya haki na sahihi kwa haraka na kuwa na uwezo wa kuyaelezea kwa maandishi au kuzungumza;

f) Uwezo wa kumudu masuala magumu yanayoleta (yenye) hisia na changamoto kwa kutumia mbinu sahihi na njia za kiplomasia;

g) Uwezo wa kushughulikia masuala na malalamiko nyeti kijamii na kisiasa kwa usiri, pale inapohitajika;

h) Ujuzi mkubwa wa kutatua migogoro; na

i) Uwezo wa kufanya kazi vizuri kama sehemu ya timu, au kama mtu binafsi (akiwa peke yake).

MAJUKUMU

a) Kuandaa na kutekeleza maamuzi ya kisera ya Tume;
b) Kuelekeza, kusimamia na kuwa mwangalizi wa kazi za Idara za Tume;
c) Kumsaidia Mwenyekiti katika kutekeleza majukumu na kazi za Tume; na
d) Kutekeleza kazi yoyote atakayopangiwa na Mwenyekiti wa Tume.

KITUO CHA KAZI

DODOMA (4), na ZANZIBAR (1)

MUDA WA AJIRA

Nafasi zote za uteuzi zitakuwa na kwa kipindi cha muda wa miaka mitatu na uwezekano wa kuteuliwa tena kwa muhula mwingine mmoja usiozidi miaka mitatu kwa kutegemea na utendaji wa kazi.

UTARATIBU WA MAOMBI

Maombi yote sharti yafanyike kwa barua iliyoandikwa kwa mkono au kuchapwa ikiambatisha Wasifu wa Mwombaji (CV), nakala zilizothibitishwa (Certified copies) za vyeti vya kitaaluma, barua za wadhamini watatu , ikiwemo namba za simu na anuani ya barua pepe ya Mwombaji na Wadhamini.

Muhimu

Watu wote waliowahi kuleta maombi katika mchakato uliopita wanashauriwa kuwasilisha maombi upya.

UWASILISHAJI WA MAOMBI

Maombi yote, ikiwemo barua zilizosainiwa za Wadhamini, zinatakiwa kutumwa kwa njia ya posta, faksi, barua pepe au kuletwa kwa mkono katika Ofisi ya Katibu wa Kamati ya Uteuzi kwa kupitia maelekezo yafuatayo hapa chini:

Katibu wa Kamati ya Uteuzi,
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
Kiwanja Na. 21,
Mtaa wa Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P 630, **DODOMA.**

Simu ya Mkononi: +255 737 103 239
Simu Namba: +255-26-2321861
Faksi: +255-26-2321681
Anuani ya barua pepe: dag@agctz.go.tz

AU

Katibu wa Kamati ya Uteuzi,
C/o Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,
Haki House, Mtaa wa Luthuli,
S.L.P 2643,
DAR ES SALAAM.

Simu ya Mkononi: +255 737 103 239
Simu Namba: +255 (022) 2135747/8, 2137125
Faksi: +255 (022) 2111281
Anuani ya barua pepe: chragg@chragg.go.tz

MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI: **8 MEI 2019, saa 10:00 jioni.**